

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

CHUO CHA ARDHI TABORA

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA NA SERIKALI KUPITIA
OR-TAMISEMI**

1. Wanafunzi wanapaswa kuchukua fomu ya maelekezo ya kujiunga na Chuo cha Ardhi Tabora ambayo inapatikana katika tovuti ya Chuo ambayo ni www.arita.ac.tz
2. Katika tovuti hiyo, mwanafunzi atapata maelekezo ya kujiunga na Chuo cha Ardhi Tabora (*Student Joining Instructions*) ambayo itaelekeza mahitaji muhimu ya mwanafunzi pamoja na ada ya masomo kwa mwaka na Hosteli.
3. Ni jukumu la Mwanafunzi na Mlezi kusoma kwa kina maelekezo ya kujiunga na Chuo ili kufanya maandalizi mapema kabla ya Chuo kufunguliwa kwa masomo ya mwaka 2022/2023.
4. Chuo kinatarajiwa kufunguliwa mwezi **Oktoba, 2022**.
5. Kwa maelezo zaidi mwanafunzi anapaswa kufuatilia matangazo kuhusu nafasi yake ya masomo kupitia tovuti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) na Tovuti ya Chuo cha Ardhi Tabora www.arita.ac.tz

Kwa mawasiliano zaidi: piga Simu Na. 026 2604591 na 0714 896425.

UTAWALA